# ACADEMIC BREAKTHROUGH SERIES

SASON 001

## DARASA LA NANE - MWAKA - 2021

## KISWAHILI : LUGHA

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

MUDA: SAA 1 DAK. 40

I) JINA LAKO II) JINA LA SHULE YAKO

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Chagua jibu linalofaa zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Mchezaji __1__ uwanjani huwa na __2__ yaani matarajio ya kupata ushindi __3__ kwamba kufanikiwa kwa mchezaji __4__ kujitolea kwake, mara nyingi ushirikiano na waelekezi wake __5__. Ama kwa kweli __6__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. anapojitoma | B. anavyojituma | C. anakojituma | D. anaojituma |
| 2. | A. hali | B. mwamka | C. azma | D. hima |
| 3. | A. fauka na | B. zaidi na | C. licha ya | D. bila ya |
| 4. | A. unategemea | B. utegemeana | C. kutegemea | D. hutegemea |
| 5. | A. unahitaji | B. unahitajika | C. huhitaji | D. kwahitajika |

6. A. jifya moja haliinjiki chungu B. mpishi mmoja walaji wengi
   C. akiba haiozi D. damu ni nzito kuliko maji

Bila shaka umewahi kusikia kwamba siku njema huonekana asubuhi? __7__ mustakabali wa __8__ ya binadamu __9__ na namna __10__ maisha yake. Binadamu lazima ajizoeshe __11__ tangu utotoni kuyatosheleza mahitaji __12__ yaani __13__ mtu wa kupakata mikono __14__ kungojea kusaidiwa. Hata itokeapo atasaidia ajikakamue kwani __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | A. Nayo | B. Nawe | C. Nawo | D. Nao |
| 8. | A. aushi | B. mwaka | C. mwenendo | D. wazo |
| 9. | A. uathiriwa | B. uadhiriwa | C. huadhiriwa | D. huathiriwa |
| 10. | A. anayoyaendesha | B. anavyoyaendesha | C. anapoyaendesha | D. anaendesha |
| 11. | A. kujizatiti | B. kujiweza | C. kujijenga | D. kujijua |
| 12. | A. zake | B. chake | C. yake | D. zao |
| 13. | A. asiwe | B. asije | C. awe | D. aje |
| 14. | A. lau | B. lakini | C. ila | D. wala |

15. A. fimbo ya mbali haiuwi nyoka B. mtoto wa nyoka ni nyoka
    C. ukibebwa usilevyelevye miguu D. akiba haiozi

***Kutoka swali la 16 - 30, chagua jibu mwafaka kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. ***Taja aina ya neno lililopigiwa mstari.***
Vitabu **vizuri** vimenunuliwa.
A. Kivumishi B. Kiwamilishi
C. Kielezi D. Nomino

17. Ni sayari ipi iliyo mbali zaidi na jua?
A. Zaibaki B. Utaridi
C. Kausi D. Zuhura

18. Neno lenye maana sawa na hasira ni
A. hadaa B. ghairi
C. ghaidhi D. ghasi

19. Idara ya msitu hupatikana katika idara gani?
A. Wizara ya elimu
B. Wizara ya fedha
C. Wizara ya misitu na maliasili
D. Wizara ya utamaduni

20. ***Chagua neno ambalo nikiunganishi katika sentensi hii.***
Mwalimu alienda darasani lakini hakufundisha.
A. mwalimu B. alienda
C. lakini D. darasani

21. ***Chagua wingi wa sentensi hii.***
Jizi hilo lilikuwa na jizu mkononi.
A. Vijizi hivyo vilikuwa na vijusu vikononi
B. Wezi hao walikuwa na visu mikononi
C. Majizi hao yalikuwa na majisu makononi
D. Majizi hayo yalikuwa na majisu makononi

22. ***Andika kinyume cha sentensi hii.***
Harufu nzuri imemtamanisha mgeni.
A. Harufu mbaya imemtamanisha mgeni
B. Harufu mbaya imemtabisha mgeni
C. Harufu mbaya imemtamanisha mgeni
D. Harufu mbaya imemtamausha mwenyeji

23. ***Andika kwa tarakimu;***
Milioni mia moja, elfu moja na moja na moja
A. 111101001 B. 101101100
C. 100101001 D. 101111001

24. ***Kamilisha methali.***
Zunguo la mtukutu ni ___________
A. ufito B. kumwepa C. jela D. dunia

25. Kiwete aliyewasili aa shahada ya uzamifu. Tumia **'amba'**
A. kiwete ambacho kimewasili kina shahada ya uzamifu
B. kiwete ambacho amesili ana shahada uauzamifu
C. Kiwete ambaye amewasili ana shahada uzamifu
D. Kiwete ambaye aliyewasili ana shahada ya uzamifu

26. ***Tambua kivumishi cha A unganifu katika sentensi hii.***
Duka la nguo na viatu ni hili.
A. na B. hili
C. ni D. la

27. ***Sahihisha sentensi hii;***
Mananasi hii inauzwa ghali kwa sababu ni mzuri sana.
A. Mananasi hii inauzwa ghali kwa sababu ni mzuri sana
B. Mananasi haya zinauzwa ghali kwa sababu ni mazuri sana
C. Mananasi haya yanauzwa ghali kwa sababu ni mazuri sana
D. Mananasi hizi yanauzwa ghali kwa sababu ni mazuri sana

28. Mwanamume huyu ametia mbugi miguuni yaani
A. hatulii kwa kwenda
B. amevaa soksi chafu miguuni
C. amejipamba
D. ametoroka kwa mguu

29. Akisami $^3/_8$ husomwa
A. theluthi tatu B. theluthi
C. thumni nane D. thumni tatu

30. Nini ukubwa wa sentensi hii?
Mbwa mweusi anamkimbiza mtu.
A. Jibwa jeusi linalikimbiza jitu
B. Jibwa cheusi linamkimbiza kijitu
C. Kijibwa kieusi kinakimbiza kijitu
D. Jibwa jeusi anakimbiza jitu

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31 hadi 40.**

Ingawa mitihani ni muhimu katika mfumo wowote ule wa elimu ni muhimu kutaja kwamba, kwa sababu ya kusisitiza umuhimu mitihani visa vingi vya udanganyifu vimeripotiwa. Baadhi ya wanafunzi hunakili majibu kutoka vitabuni ili kupita mitihani yao ya shule ya upili au chuo kikuu. Wavyele wengine huwalipa watu fulani kuwafanyia watoto wao mitihani. Hivi ni vitendo visivyokubalika. Kila mwaka matokeo ya mtihani yanapotangazwa, hatukosi kusikia kuwa shule

fulani haikupata matokeo kwa sababu ya visa vya undanganyifu. Hali inapokuwa hivyo wanafunzi husika hulazimika kurudia mtihani baadaye. Huu ni ubadhirifu wa mali na wakati.

Hali kadhalika, mitihani japo hupima uwezo wa mwanafunzi katika masomo fulani hauwezi kutumiwa kama kigezo tosha cha kutathmini umilisi wa mwanafunzi. Wapo baadhi ya wanafunzi ambao ni hodari masomoni lakini huenda wasifanye vyema katika mtihani. Jambo hili huweza kusababishwa na hali ya afya ya mwanafunzi wakati wa mtihani, na fadhaa au uchechefu wa karo. Baadhi ya watu ambao hawakufua dafu katika mitihani huenda wakawa watenda kazi wema.

Mitihani huhitaji matayarisho ya dhati. Mwalimu pia ana jukumu la kumsaidia mwanafunzi katika kujitayarisha kwa kuhakikisha kuwa amemwelekeza kuhusu jinsi ya kukabiliana na aina mbalimbali za maswali na jinsi ya kuutumia muda wake. Aidha, anastahili kumshauri ni somo gani linalohitajika kushughulikiwa kwa makini zaidi. Aidha, amshauri mwanafunzi kuhusu jinsi ya kudurusu na kujihusisha katika michezo ili kupumzisha ubongo. Bila kusahau ni muhimu mwanafunzi kujua kwamba anahitaji lishe bora ili kupata nguvu ya kuyatalii masomo na kuikabili mitihani yake.

Binadamu hana budi kufanya mitihani mbalimbali uashini mwake. Hata hivyo haifai kuichukua mitihani kama kibali cha kuwabagua watoto. Baadhi ya wanajamii huwadharau wale wasiofaulu katika mitihani na katika masomo yanayostahiwa na jamii. Watoto huingiwa na kiwewe na hukosa kujiamini. Aidha, wazazi wengine huwalazimisha watoto wao kuzisomea taaluma ambazo wao wazazi wanazipendelea. Mwishowe huishia kufanya masomo wasiyioyamudu barabara. Wanaofanya vyema hushehenezwa sifa belele mbele ya ndugu zao pasi kujali hisia za umbu wao. Hii husabanisha uhasama miongoni mwa ndugu. Uhasama huu huenda ukaleta hasara. Hatuna budi kuitumia mitihani kwa kumkuza binadamu bali si kumviza.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
A. umuhimu wa mitihani huchangia udanganyifu
B. utiliaji mkazo katika umuhimu wa mitihani huchangia udanganyifu
C. wote wanaofua dafu hawana budi kudanganya
D. mitihani ndiyo njia ya pekee ya maendeleo

**32.** Upi si udanganyifu katika mitihani?
A. Kudurusu kabla ya mtihani
B. Kufanyiwa mtihani na mtu mwingine
C. Kuangalia majibu vitabuni wakati wa mtihani
D. Kunakili majibu kutoka kwa wanafunzi wengine

**33.** Madhara makuu ya udanganyifu wa mtihani ni
A. kupata matokeo duni kwa sababu ya ujanja
B. kufungwa jela kwa wadanganyifu
C. matumizi mabaya ya mtihani
D. kupigwa marufuku kwa shule na kurudia mtihani

**34.** Kwa nini mtihani si kigezo bora cha kupimia umilisi?
A. Huwachosha watahiniwa
B. Huku ni kuwaapuuza wale dhaifu katika masomo
C. Mitihani huchukua wakati mwingi
D. Yapo maswala yanayowaathiri hata wale wanafunzi hodari wakafeli

**35.** Neno kiwewe lina maana sawa na
A. furaha  B. hasira
C. wasiwasi  D. kicheko

**36.** Jukumu kuu la mwalimu katika mtihani ni
A. kuteua majibu sahihi ili kumsaidia mwanafunzi
B. kumtamausha mwanafunzi kabla ya mtihani
C. Kumwandaa mwanafunzi kikamilifu kabla ya mtihani
D. Kumshauri na kumghilibu mwanafunzi kuhusu kunakili majibu

**37.** Huenda mwanafunzi mwerevu akakosa kufanya vyema katika mtihani kwa sababu ya
A. Afya njema wakati wa mtihani
B. Kudurusu kidogo tu kabla ya mtihani
C. Kutokuwa na karo
D. Kufanya bidii wakati wa mtihani

**38.** Ni kweli kusema kuwa
A. watu wote waliofeli mtihani wameshindwa kufanya kazi njema
B. baadhi ya watu hujiangusha katika mtihani ili wapate kazi njema
C. kwa kiwango fulani, mtihani imesababisha migogoro katika familia
D. Waliofeli mtihani walirudia na kuifanya vyema

39. Kulingana na aya ya tatu;
A. michezo haifai katu, tutafute vigezo vingine
B. Lishe bora husaidia kumpumzisha akili
C. Michezo huleta nguvu za kuyatalii maswali
D. Lishe bora huvinyosha viungo vya mwili

40. Mwandishi wa makala haya anaonelea kuwa;-
A. mitihani haifai tutafute vigezo vingine
B. mtihani unaweza kumkuza au kumviza mtu
C. mitihani inafaa sana kama kigezo cha kutathmini masomo
D. ni muhali kukabiliana na udanganyifu katika mitihani

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50.</u>***

Naichukua fursa hii kutatama kwa fasili na kinagaubaga mbinu mbalimbali ambazo mwanafunzi anaweza kuzitumia katika kujifunza na kuelewa lugha ya Kiswahili akiwa shuleni.

Ili afaulu sharti mwanafunzi awe na vitu vifuatavyo. Bidii katika kujifunza Kiswahili, nia au **<u>ari</u>** ama hamu na ghamu ya kutaka kuielewa lugha ya Kiswahili. Hatimaye awe na ukweli au uhakika wa mambo anayojifunza kuhusiana na lugha hii.

Aidha ningependa mporomoko wangu wa shukurani za dhati zisizokuwa na mizani ziwafikie walimu wa wanafunzi wote wanaojitolea kufa kupona kujifunza na kukuza Kiswahili kwa hali na mali, usiku na mchana. Kwa juhudi zao nyingi kama za mchwa wanaojenga kichunguu kwa mate katika gogo la hazari, wamekiwezesha kiswahili kupanda na kupanuka kiasi cha kufikia bora unaothaminika. Billahi! penye nia pana njia, aidha umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

41. Mwanafunzi awe na nini anapojifunza Kiswahili?
A. Nia B. Nguvu
C. Uhakika D. Nidhamu

42. **<u>Ari</u>** inamsaidia vipi mwanafunzi katika kujifunza?
A. Asikate tamaa
B. Aelewe haraka
C. Aongee kwa ufasaha
D. Kupata njia

43. Neno **<u>fursa</u>** ni sawa na
A. furaha B. saa
C. wasaa D. ruhusa

44. Kiswahili ni lugha ya kiafrika inayozungumzwa zaidi kati nchi ya Afrika mashariki na kati asili ya Kiswahili ni
A. kiarabu
B. kimombo
C. kizungu
D. kikoloni

45. **<u>Aidha</u>** ni sawa sawa na ____________
A. vilevile B. wingi wa mawaidha
C. aidha D. sasa

46. Neno kukuza ni mnyambuliko wa
A. kula B. kuwa
C. kua D. kulia

47. Wanafunzi wanaojitolea husaidia
A. kuimarisha Kiswahili
B. kudunisha Kiswahili
C. kukuza mali
D. kuwafunza wengine

48. Bidii za mchwa humithilishwa na za watu
A. wanaozembea kazini
B. wanaopenda kazi
C. hodari
D. wafanyao kazi bila kuchoka

49. Kinyume cha usiku ni mchana. Kinyume cha juhudi ni
A. ugoigoi B. bidii
C. uchovu D. upole

50. Kwa jumla habari hii ni juu ya
A. Kutimiza mtaala wa Kiswahili
B. Kuwashutumu wazembe wa Kiswahili
C. Kuwashukuru wasomi
D. Kufafanua mbinu za kukifahamu Kiswahili